



Picha kwa hisani ya TCCIA

## SAUTI ZA WATANZANIA – CHUNGUZI KIFANI JUU YA BIASHARA NA HAKI ZA BINADAMU (TOLEO LA 3): “ATHARI ZA MIRADI MIKUBWA YA MIUNDOMBINU KWA HAKI ZA BINADAMU”

### Swahili summary

Toleo hili la tatu la “Sauti za Watanzania” linaelezea tafti kwa kujikita kwenye “**athari za miradi mikubwa ya miundombinu kwa haki za binadamu**”, kama ilivyofanywa na Shirika la Maendeleo ya Gesi (PILIDO), Asasi ya Governance Links Tanzania, Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA), Msingi wa Usimamizi wa Mazingira na Kampeni dhidi ya Umaskini (FEMAPO) na Asasi ya Kutetea Haki katika Jamii (AJISO). Uhariri umefanywa na Shirika la IPIS.

## UTANGULIZI

Tangu aingie madarakani mwaka 2005, Rais Magufuli ametilia mkazo kwenye **maendeleo ya miundombinu kama jambo muhimu katika kufikia malengo ya Tanzania ya viwanda na maendeleo**. Alisema waziwazi kwamba “*Kama unataka kukua kiuchumi, wekeza kwanza kwenye miundombinu ambayo itachochea ukuaji*”<sup>1</sup>. Matokeo yake, miradi mingi ya miundombinu mikubwa ipo na imekuwa ikiendelea kuwepo nchini, kuleta miundombinu ya barabara, mukarabati wa mifumo ya reli na viwanja vya ndege, na kuongeza usambazaji na kuwa na aina nyingi ya nishati nchini kupitia mitambo ya gesi asilia na umeme wa maji, kwa kutaja tu kwa uchache<sup>2</sup>.

Wakati ambapo miradi ya miundombinu inaleta maendeleo chanya, ajira na ukuaji wa uchumi, upanuzi wa haraka wa sekta unaleta pia **athari hasi kwa jamii na mazingira** ambamo miradi inatekelezwa au kwa wanaojihusisha na utekelezaji wa miradi hii. Mwaka 2017, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), kupitia Tathmini yake ya Awali ya Kitaifa juu ya utekelezaji wa sasa wa Mfumo wa Biashara na Haki za Binadamu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<sup>3</sup>, ilidokeza uhitaji wa kuzingatia haki za binadamu kwenye sekta ya ujenzi inayokua kwa kasi nchini. Tangu wakati huo, wasiwasi juu ya athari za miradi kadhaa maarufu ya miundombinu nchini Tanzania imebuliwa na mashirika yasiyo ya kiserikali<sup>4</sup>. Uchunguzi kifani juu ya masuala ya haki za binadamu wakati wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, uliochapishwa na toleo la kwanza la “*Sauti za Watanzania*”<sup>5</sup>, unaeleza kwa kina juu ya kiwango cha jinsi kazi za miundombinu zinaweza kugusa haki za msingi, za binadamu duniani. Hizi ni pamoja na haki za ardhi, kupata haki, masharti ya kazi na ajira, kiwango bora cha maisha, ushiriki wa jamii, haki za makundi ya wenyeji na haki za mazingira.

- 1 Magufuli akingia kifua miradi ya miundombinu. The Citizen; 05.09.2020. <https://www.thecitizen.co.tz/news/Magufuli-defends-big-infrastructure-projects/1840340-5619578-w1hbg/index.html>
- 2 Muhtasari wa kazi za miundombinu za hivi karibuni nchini Tanzania zinaweza kupatikana katika mfululizo wa “Biashara na Haki za Binadamu nchini Tanzania”: <https://ipisresearch.be/briefings/tanzania-briefing/>
- 3 Tathmini ya Awali ya Kitaifa (NBA) ya utekelezaji wa sasa wa mifumo ya biashara na haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. CHRAGG, DIHR & SOMO; Novemba 2017. <https://globalnaps.org/country/tanzania/>
- 4 Angalia k.m. [https://www.panda.org/wwf\\_news/press\\_releases/?340151/Tanzania-signs-contract-with-Egypt-to-build-controversial-hydroelectric-dam-in-UNESCO-World-Heritage-site-Selous](https://www.panda.org/wwf_news/press_releases/?340151/Tanzania-signs-contract-with-Egypt-to-build-controversial-hydroelectric-dam-in-UNESCO-World-Heritage-site-Selous) or <https://oxfamlibrary.openrepository.com/bitstream/handle/10546/621045/rr-empty-promises-down-line-101020-en.pdf?sequence=1&isAllowed=y>
- 5 <https://ipisresearch.be/publication/voices-tanzania-case-studies-business-human-rights-vol-1/>

Vipengele vya haki za binadamu mara nyingi hupuuza kwenye shughuli za biashara<sup>6</sup>. Ili kukuza usimamizi wa haki za binadamu na sekta ya biashara, Umoja wa Mataifa ulitunga **Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu**, yaani UNGPs<sup>7</sup>. Wakati UNGPs inasema wazi kuwa ni jukumu la Serikali *kulinda* raia dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu mahali pa kazi (Nguzo ya I ya UNGP), inaonyesha pia kwamba makampuni yana jukumu la *kuheshimu* haki za binadamu (Nguzo ya II ya UNGP). Hii inamaanisha kwamba yanapaswa kuchukua hatua ya dhati ili kuepuka kukiuka haki za binadamu. Michakato ya **utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu** – yaani, hatua zote muhimu za kutambua, kuzuia, kupunguza na kuhesabu athari hasi za haki za binadamu zinazohusiana na shughuli<sup>8</sup> - kwa sasa ni michakato ya hiari na makampuni binafsi. Hata hivyo, kasi inakua duniani kote na kufanya utekelezaji wa haki za binadamu kuwa wa lazima katika minyororo (fulani) ya ugavi au viwanda<sup>9</sup>. Nchini Tanzania, bado hakuna mfumo maalum wa sheria ambao unalazimisha makampuni kutekeleza haki maalum za binadamu. Pamoja na hilo, kuna mahitaji ya lazima ya kutathmini kama mradi wa biashara umeshughulikia vya kutosha na kwa ufanisi athari zake (tarajiwa) za mazingira na za kijamii na kama kuna kupunguza kwa dhati athari hizo<sup>10</sup>. Je, mahitaji haya yanatosha kuweka wazi masuala yote ya haki za binadamu yanayohusiana na shughuli zinazoongezeka za biashara nchini? Na hali ya sasa, asili na ukubwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu mahali pa kazi na hatari kuhusiana na maendeleo ya miundombinu ikoje? Kama taarifa juu ya mada hizi ni za kutisha wakati sekta inaendelea kukua, miradi mikubwa ya miundombinu inahitaji umakini wa dharura kwa kujikita kwenye mtazamo wa haki za binadamu.

## CHUNGUZI KIFANI

Tafti juu ya *“Sauti za Watanzania”* zimebuniwa kama tafti ndogo ndogo, za uwandani, zilizofanywa na asasi za kiraia nchini Tanzania, zinazokusudia kumulika masuala yanayohusu **biashara na haki za binadamu nchini Tanzania**. Kupitia uwepo na shughuli zao, makampuni yanaweza kuwa na nafasi kubwa katika kukuza na kuminya haki za binadamu.

Tafti juu ya *“Sauti za Watanzania”* zinahusisha **data za uwandani**, zilizopatikana kupitia k.m. usaili kwa wadau, ushuhudiaji au hojaji, na vyanzo vya data za upili kama vile mifumo ya sheria za ndani (na za kimataifa), ripoti zilizochapishwa au nyaraka (sera) za makampuni. **Uchambuzi** wake unawasilisha taarifa ambazo zilikuwa hazijachapishwa hapo awali, unatoa uelewa mpya na **mapendekezo ya wazi** kwa wadau mbalimbali wanaohusika.

Mfululizo huu wa tafti juu ya *“Sauti za Watanzania”* ulifanywa wakati wa **janga la Uviko-19**, ambalo lilileta changamoto maalum wakati wa ukusanyaji wa data na kuwafikia wadau. Ili kupunguza safari na kukutana ana kwa ana, data mpya zilipatikana kwa mbali, kupitia mahojiano ya simu moja kwa moja na wadau au wahusika wa eneo. Tafti nyingine zinategemea sana data zilizokusanywa hapo awali ambazo zilihitaji ufuatiliaji au maboresho madogo madogo.

Toleo la tatu la *“Sauti za Watanzania”* linaelezea **chunguzi kifani tano zinazojikita kwenye athari za miradi mikubwa ya miundombinu kwa haki za binadamu**. Tafti hizo zilitathmini athari za haki za binadamu kwenye **miradi mitatu ya usambazaji wa nishati**– Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (mkoa wa Manyara), Mradi wa Umeme wa Maji wa Maporomoko ya Rusumo (mkoa wa Kagera) na miradi ya usambazaji wa nishati vijijini (mkoa wa Mwanza) – na **miradi miwili inayohusu miundombinu ya uchukuzi** –mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania (mikoa ya Arusha na Dodoma) na reli ya Dar es Salaam - Moshi (mkoa wa Kilimanjaro).

6 Angalia k.m. <https://www.corporatebenchmark.org/2020-results>

7 Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji wa Mfumo wa ‘Kulinda, Kuheshimu na Kupata Unafuu wa Kisheria’, Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR); 2011. [https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR\\_EN.pdf](https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR_EN.pdf)

8 <https://www.ohchr.org/EN/Issues/Business/Pages/CorporateHRDueDiligence.aspx#:~:text=Human%20rights%20due%20diligence%20is,with%20which%20they%20are%20involved.&text=The%20prevention%20of%20adverse%20impacts,people%2C%20not%20risks%20to%20business.>

9 Kwa muhtasari juu ya Ulaya, angalia: <https://www.business-humanrights.org/en/latest-news/national-regional-movements-for-mandatory-human-rights-environmental-due-diligence-in-europe/>

10 K.m. Matakwa ya Tathmini ya Athari za Mazingira na za Kijamii (ESIA) kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004

Tafti hizi ziliongozwa na maswali yaliyohusu:

1. **utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu** unaotakiwa kufanywa na makampuni: makampuni yanafanya nini katika kuheshimu haki za binadamu, kuzuia ukiukwaji wa haki za binadamu na kupunguza athari mbaya?
2. **athari** za miradi maalum ya miundombinu **kwa jamii**: ni nini athari halisi au zinazotarajiwa kwa jamii kama ilivyozoeleka, na zinahusiana vipi na hatua zozote zinazochukuliwa na makampuni za kuzuia / kupunguza hizo athari?
3. **upatikanaji wa fidia endapo kuna ukiukwaji wa haki za binadamu**: kuna njia na taratibu zilizowekwa kwa watu kutoa kero zao na kupata fidia sahihi kutokana na athari mbaya, kama zitatokea?
4. **uhusishwaji, ushiriki na uhamasishwaji** wa jamii **katika maendeleo ya miundombinu na haki za binadamu**: ni kwa vipi (kiasi gani) jamii zilihusishwa katika kubuni, tathmini, utekelezaji na upunguzaji wa athari katika miradi ya miundombinu?



*Maelezo ya jumla ya tafti tano zilozajumuishwa kwenye chapisho la "Sauti za Watanzania – chunguzi kifani juu ya Biashara na Haki za Binadamu (Toleo la 3)"*

**Shirika la Maendeleo ya Gesi (PILIDO)** linawasilisha tathmini ya jinsi mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) utakavyoathiri haki za binadamu na maisha ya jamii za wafugaji na wakulima katika Wilaya ya Kiteto, mkoa wa Manyara. Jamii za wafugaji / wakulima na wafugaji, wenyeji wa eneo hili, wanategemea ardhi na maliasili kwa ajili ya maisha endelevu. Athari zisipopunguzwa vya kutosha, ujenzi wa bomba linalopita chini, lenye joto katika eneo hilo lina uwezo wa kuongeza mahitaji makubwa ya rasilimali ambazo tayari hazitoshi na tayari kuna tishio la kukosa mikakati ya kukabiliana na viwango vya mahitaji ambavyo haviwezi kutosheleza jamii hizi.

**Asasi ya Links Governance Tanzania** ilichunguza ni kwa kiasi gani sehemu ya Tanzania ya Mradi wa Umeme wa Maji wa Maporomoko ya Rusumo inatekeleza haki za binadamu. Ili kuongeza uzalishaji wa nishati katika mkoa, kituo cha umeme cha Megawati 80 na miundombinu inayohusiana kimejengwa karibu na maporomoko ya Rusumo katika Wilaya ya Ngara, mkoa wa Kagera. Huko, takribani watu 39,000

wameathiriwa na mradi huo na kwa mantiki hii, athari kwa haki zao za binadamu kiuchumi, kimazingira, kijamii na kiutamaduni zinahitaji ufuatiliaji.

**Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA)** kimechapisha utafiti kuhusu athari za haki za binadamu kwa wafanyabiashara wanaotekeleza miundombinu ya usambazaji wa umeme katika wilaya mbili za vijijini za mkoa wa Mwanza (Wilaya za Misungwi na Kwimba). Huko, nyumba nyingi hazijaunganishwa kwenye gridi ya umeme na upatikanaji wa umeme una uhakika wa kuleta maendeleo chanya. Mbali na muhtasari wa athari, utafiti pia unatoa mwanga juu ya mwamko wa utekelezaji wa haki za binadamu na makampuni, mamlaka za mitaa na wanajamii ambako maendeleo ya miundombinu yalitokea.

Utafiti uliofanywa na **Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Kampeni dhidi ya Umaskini (FEMAPO)** ulichunguza utekelezaji wa haki za binadamu na ushiriki wa raia katika utekelezaji wa Mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania katika miji miwili ulipofanyikia mradi, Arusha na Dodoma. Mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania ni mradi mkubwa wa maendeleo ya miundombinu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambayo ililenga kuboresha miundombinu na huduma za miji katika miji minane inayokua kwa kasi nchini Tanzania. Wakati mradi huo utaleta maendeleo na usalama unaohitajika kwa viunga vya miji, haki za binadamu zinatakiwa kuzingatiwa katika utekelezaji wake ili kuhakikisha kunakuwa na mabadiliko chanya na hali bora kwa jamii.

Kama utafiti wa tano na wa mwisho katika toleo hili la tatu, **Asasi ya Kutetea Haki katika Jamii (AJISO)** inawasilisha kesi inayohusiana na ukarabati wa reli ya Dar es Salaam-Moshi na athari zake kwa jamii za Wilaya za Mwanga na Moshi, mkoa wa Kilimanjaro. Kama ilivyo miradi mingine ya miundombinu, kazi za ukarabati zinaweza kuleta athari chanya na hasi kwa haki za kimsingi za binadamu kama vile haki za wafanyakazi, haki ya kuishi kwa usalama na afya njema na haki za mazingira. Kwa hiyo AJISO ilitathmini ni kwa kiwango gani mradi huu wa miundombinu ulizingatia viwango vya haki za binadamu, na hasa Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu.



### Athari za Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa Haki za Binadamu na Mazingira kwa Jamii za Wakulima na Wafugaji katika Wilaya ya Kiteto, Manyara, Tanzania (PILIDO)

*Utafiti huu mdogo wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), unatathmini athari za mradi huu mkubwa wa miundombinu juu ya haki na maisha ya jamii za wafugaji na wakulima katika Wilaya ya Kiteto, mkoa wa Manyara, kaskazini mashariki mwa Tanzania. EACOP ni mradi wa miundombinu ya serikali kuu ya Uganda na Tanzania, ambayo itasafirisha mapipa 216 ya mafuta ghafi kwa siku kutoka Kabaale, wilayani Hoima (magharibi mwa Uganda) hadi Rasi ya Chogoleani karibu na bandari ya Tanga (mashariki mwa Tanzania). Ukikamilika, itakuwa bomba refu zaidi lenye joto ulimwenguni (km 1,443).*

Nchini Tanzania bomba linapita katika mikoa 8, wilaya 24, kata 116 na vijiji 231 kwa umbali wa kilomita 1,147. Kwa hivyo EACOP inavuka mifumo anuwai ya kiikolojia, mito, nyanda za juu, ardhi kame na maeneo ya uhifadhi, pamoja na jamii nyingi za wafugaji na wakulima. Wakati mradi huo utaleta mapato muhimu kwa watengenezaji wa kimataifa na serikali, athari za mazingira kwa maisha ya jamii za wafugaji na wakulima zinaonekana.

Katika Wilaya ya Kiteto, EACOP itachukua kilomita 113 na itaathiri vijiji 7 vya Mutikira, Ndorkon, Ndaleta, Orpopong'i, Kimana, Amei, na Loolera. Vijiji vinne kati ya hivi - Ndorkon, Amei, Orpopong'i na Loolera - ndio lengo la utafiti huu. Jamii za wafugaji / wakulima-wafugaji ni za asili katika eneo hilo, na hutegemea ardhi na maliasili kupata maisha endelevu. Kwa zaidi ya miaka 40, jamii zimepata hasara ya mali hizi muhimu, haswa ardhi, kwa miradi ya uwekezaji na mabadiliko ya hali ya hewa, na hivyo kuhatarisha haki yao ya maisha bora. EACOP itaongeza shinikizo juu ya rasilimali zilizopungua na mikakati ya kukabiliana na wafugaji, na hivyo kuongeza tishio kwa haki za kimsingi za jamii za wafugaji kwa maisha bora. Changamoto za EACOP kwa haki za binadamu na mazingira zinahitajika kutathminiwa

Utafiti huu unakusudia kutathmini athari za EACOP kwa haki za kijamii na kiuchumi, binadamu na mazingira katika vijiji 4 vya wilaya ya Kiteto, kuongeza uelewa juu ya masuala yanayokabiliwa na jamii za wafugaji na wakulima katika miradi mikubwa ya miundombinu na kushiriki mapendekezo juu ya jinsi ya kukuza na kulinda haki za binadamu katika vijiji vilivyoathirika. Maswali muhimu ya utafiti kwa hivyo ni: (1) Je! Haki za kijamii na kiuchumi, binadamu na mazingira zinaathiriwa vipi na mradi wa EACOP? na (2) EACOP inafanya nini kupunguza hatari hizi na hii inatosha?

Utafiti huu ulitumia njia za kukusanya taarifa kwa mapitio ya dodoso, maswali na ajadiliano katika vikundi na mahojiano kwa jina ya simu .

Katika utafiti huu, tuligundua kuwa jamii inaogopa kupoteza maeneo yao ya malisho pamoja na maeneo yao ya makazi pia kuna uwezekano wa upotevu wa amani na ustawi, maisha hasa utamaduni wao kutokana na muingiliano wakati utafiti huu wa EACOP ukitathimini athari hizi na athari zipatipatikanazo na mradi huu EACOP imekuja na majumuisho yafuatayo

Watu wa jamii hii hawana elimu na uwelewa wa kina juu ya eneo la utafiti, hasa athari zitazoikumba jamii na maisha yao kwa ujumla. Bila mipango madhubuti kutoka kwenye jamii husika wako katika hatari ya kupoteza mifugo yao ambayo ndio tegemeo kubwa katika maisha ya ujumla ya wafugaji. EACOP itasababisha upotezaji mkubwa wa mali na ni vigumu kwa wafugaji hawa kuzoea aina nyingine mbali na ufugaji kutokana na hali ya kijiografia katika maeneo haya.

Pili, ushiriki wa wadau, mashauriano na upashanaji wa habari unaonekana kuwa hautoshi. Hakuna na mawasiliano yoyote rasmi ya kuwaelimisha watu na jamii zilizoathiriwa baada ya mikutano ya awali mnamo 2017. Uelewa wa watu kuhusu EACOP unaonekana kutotosheleza na hawana maarifa kamili juu ya ujenzi wa bomba, upunguzaji, mipango ya fidia, wala jinsi mradi huo utathiri maisha yao. Ukosefu huu wa habari na mashauriano umeibua maswali ambayo hayana majibu yalio rasmi, wasiwasi mkubwa ndani ya jamii.

Utafiti huo unahitimisha kuwa EACOP ina mipango ya kina ya usimamizi na kushughulikia athari za mradi. Mipango hii, hata hivyo, inapaswa kuwekwa kimuktadha na kubadilishwa kulingana na hali ya eneo hilo, na kuwasilishwa kwa njia ya uwazi kwa wadau wote. Shida na changamoto zinazoonekana na utekelezaji, upunguzaji na ufuatiliaji ni uwezekano ikiwa mashauriano mapana ya jamii na uwenezwaji wa maarifa uchukuliwe kwa uzito, na imani ijengwe kwa wananchi juu ya bomba hili.

Kwa hivyo tunapendekeza mapendekezo yafuatayo kwa EACOP kwa miradi mikubwa ya miundombinu:

- Kukuza na kulinda usalama wa umiliki wa ardhi na upangaji wa matumizi ya ardhi unahitajika sana, haswa kati ya jamii za wafugaji na wakulima. Maisha yanayohusiana na ardhi yanapaswa kuzingatiwa wakati wa utwaaji wa ardhi na inapaswa kuwa sehemu ya mipango madhubuti ya ufuatiliaji wakati wa utekelezaji wa miradi ya uwekezaji.
- Elimu ya kutosha juu ya uharibifu wa mazingira na upotezaji wa makazi zinapaswa kutolewa. Zinapaswa kutolewa kwa muktadha maalumu na kuhusisha jamii kikamilifu.
- Jamii zinapaswa kuhakikishiwa ustawi na usalama wa mali, tamaduni pamoja na mila na desturi zao.
- Njia za fidia kwa mali zilizopotea, rasilimali na fursa zinapaswa kuwa za kutosha na hesabu zinapaswa kusasishwa.
- Ushauri wa Umma na Utangazaji wa Umma wa habari unapaswa kuboreshwa ili kuhakikisha ushiriki na uelewa mkubwa wa jamii. Miradi ya Ugavi wa Nishati inapaswa kuzingatia athari zao katika mabadiliko ya hali ya hewa.

Tunapendekeza serikali na wawekezaji binafsi kuwekeza katika miradi mbadala, endelevu ya usambazaji wa nishati mbadala.

UTAFITI WA 2:



**Athari za Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Maji wa Maporomoko ya Rusumo kwa Biashara na Haki za Binadamu katika Wilaya ya Ngara – Kaskazini Magharibi mwa Tanzania (Governance Links)**

*Maporomoko ya Rusumo kwenye mto Kagera, yapo mpakani kati ya nchi za Rwanda na Tanzania, kiasi cha kilomita 25 kutoka eneo linalounganisha Burundi, Rwanda na Tanzania. Hapo ndipo mradi wa umeme wa Rusumo unajengwa kusaidia kupunguza upungufu wa umeme katika nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania. Mradi huu unahusisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha megawati 80 na njia tatu zitakazounganisha mitambo ya uzalishaji na gridi za mataifa hayo. Mradi huu upo katika makutano ya mpaka wa nchi hizi tatu. Katika Tanzania, shughuli nyingi za mradi zinafanyika wilayani Ngara mkoani Kagera.*

Sehemu kubwa ya wilaya ya Ngara ni maeneo ya vijijini, inayokadiriwa kuwa na idadi ya watu 401,900. Zaidi ya asimilia 80 ya wakazi ni wakulima wa kilimo cha kujikimu. Kiasi cha wakazi 39,300 ambao ni sawa na kaya 8,360 wameathiriwa moja kwa moja na mradi ( watu 16,200 in kutoka Kijiji cha Rusumo na watu 23,100 kutoka Kijiji cha Kasulo).

Lengo kuu la utafiti huu ilikuwa kuangalia jinsi ambavyo mradi wa umeme wa kikanda katika maporomoko ya maji ya Rusumo unazingatia kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu ya biashara na haki za binadamu (UNGPs), na hususani uchambuzi wa kina kuhusu kuzingatwa kwa haki za binadamu. Utafiti huu ulifanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilifanyika mapema Februari 2020 na ilihusisha watafiti kuongozwa kutembelea eneo la mradi huko Rusumo na kufikia vijiji vinane vinavyozunguka eneo la mradi. Awamu ya pili ilifanyika kati ya Juni na Julai 2020 kwa kufanya mawasiliano na makundi mbalimbali ya wadau kwenye eneo la mradi. Utafiti huu ulitumia mbinu mseto za utafiti kupata taarifa na ushuhuda kwa kuzingatia njia za kujikinga na ugonjwa wa Corona (COVID-19).

Kwa ujumla, athari ya mradi huu kwenye masuala ya haki za binadamu imeonekana zaidi katika masuala ya kiuchumi hasa haki za umiliki na matumizi ya ardhi pamoja na fursa za kuendesha maisha ya jamii. Athari hizi zilishugulikiwa kikamilifu na mradi na wale walioathiriwa walionyesha kuridhishwa na fidia iliyotolewa. Pamoja na mradi kuonyesha kuwa na mchango chanya katika kuongeza ajira na fursa za biashara, athari hasi kuhusiana na afya na mazingira zilionekana kutoshughulikiwa kikamilifu

Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa ujenzi wa mradi wa kikanda wa kufua umeme katika maporoko ya maji ya Rusumo ulipitia mchakato wa tathimini ya Benki ya dunia katika masuala ya mazingira na kijamii. Kwa mwenendo huo, mradi pia kwa kiasi fulani ulizingatia michakato mbalimbali ya kuthibitisha uchunguzi wa haki za binadamu kama inavyopendekezwa na mwongozo wa kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu masuala ya biashara na haki za binadamu. Mradi ulibainisha madhara mbalimbali yanayoweza kujitokeza na kuchukua hatua za kuyazuia. Hata hivyo, mapungufu yamebainishwa katika hatua za kupunguza madhara na utoaji wa taarifa za kushughulikia madhara hayo.

Mradi huu wa kikanda wa kufua umeme katika maporomoko ya maji ya Rusumo unatoa fursa ya kujifunza juu ya majukumu ya makampuni katika kuzingatia mwongozo wa kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu biashara na haki za binadamu (UNGPs). Ushauri kutokana na matokeo ya utafiti ni kama ifuatavyo:

1. Mradi huu wa kikanda wa kufua umeme katika maporomoko ya maji ya Rusumo ni fursa na sehemu muhimu ya kujifunza kihalisia kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) na taasisi nyingine za usimamizi kuharakisha ufahamu wa kanuni za umoja wa mataifa kuhusu biashara na haki za binadamu miongoni mwa wadau nchini Tanzania.
2. Ni muhimu kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) ikiwa ni taasisi iliyo msitari wa mbele kusaidia mamlaka ya serikali za mitaa kuelewa mbinu za kushirikisha makundi ya wadau mbalimbali katika ufuatiliaji wa kuzingatia masuala ya biashara na haki za binadamu.

3. Ni muhimu kuwa na mtazamo wa “Serikali jumuishi” katika kushirikisha vitengo mbalimbali vya makampuni yanayojishughulisha na miradi ya miundombinu kutekeleza hatua stahiki za uchunguzi kuoanisha na kanuni za Umoja wa Mataifa katika biashara na haki za binadamu na ufuatiliaji wa utekelezaji.
4. Pamoja na kutokuwapo kwa mwongozo wa kitaifa juu ya sekta ya biashara kuzingatia haki za binadamu, ni vema makampuni na mitandao yao kutumia mbinu za uchunguzi wa utekelezaji kamilifu wa kanuni za uadilifu na makubaliano ya kimkataba kama njia ya kuanza kuoanisha utendaji na mwongozo wa umoja wa mataifa.
5. Kukua kwa uwekezaji katika miradi mikubwa ya miundombinu nchini kunaashiria uhitaji wa haraka wa mwongozo wa kitaifa kuhusu biashara na haki za binadamu ukioanishwa na kanuni za umoja wa mataifa kuhusu biashara na haki za binadamu



### UTAFITI WA 3

#### **Athari za miradi mikubwa ya miundombinu kwa Biashara na Haki za Binadamu: uchunguzi kifani juu ya usambazaji wa nishati katika jamii za vijiji vya Mwanza, Tanzania (TCCIA)**

*Tafti hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya usambazaji umeme iliopo vijijini katika wilaya za Misungwi na Kwimba mkoani Mwanza. Tathnini hii inalenga kupata taarifa juu ya utekelezaji na usimamizi wa haki za binadamu jinsi unavyozingatiwa na makampuni yasimikayo miundombinu ya nishati ya umeme katika vijiji vine vya Fella, Mapilinga wilayani Misungwi na Shilanona, Isagala wilaya ni Kwimba. Kukosekana kwa taarifa za kutosha juu ya utekelezaji dhaifu wa haki za binadamu wa kampuni hizo za usimikaji miundombuni hivo imepelekea kufanya tafti ndogo ili kuhakiki uwepo wa jambo hili na hatimaye kupaza sauti. Tafti hii pia inalenga kupata majibu ya maswali yafuatayo: 1) Ni*

*kwa kiasi gani makampuni yanayotekeleza miradi ya nishati yanazingatia haki za binaadamu katika nyakati wa utekelzaji wa shughuli zao? 2) ni kwa kiasi gani pia wakazi wa maeneo ya utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini wana ufahamu juu ya haki za binadamu na ni kwa kiasi gani haki hizo zimefunjwa na makampuni hayo? 3) na Je wakazi wa maeneo hayo wanajua taratibu za kufikisha mashtaka ili yapatiwe ufumbuzi, je taratibu hizo zipo, na kama zipo je wanazijua?*

Tafti hii ndogo, imegundua yafuatayo; 1) makampuni mengi yanayotekeleza miradi ya umeme au nishati hayazingatii haki za binadamu wakati wa kupanga na wakati wa utekelezaji, 2) kuna mambo kadhaa yaliojitokeza nayo ni kama vile, maswala ya rushwa, haki za wafanyakazi, utaratibu mbaya wa kurejesha malipo ya ardhi (fidia). 3) hata hivyo tafti hii pia imeonyesha kuwa kuna kiwango kikubwa cha wanainchi kutokua na ufahamu juu ya haki za binadamu na madhara yake, na 4) pia hakuna utaratibu muafaka unaowawezesha watu kupata suluhu juu ya madhara yanayojitokeza na hakuna namna ambayo wanainchi wanaweze kupata haki kwa kusaidiwa na makampuni hayo, kwakua hata hao wenye kutekeleza shughuli hiyo pia hawajui wajibu wao. Kwa ujumla ni kwamba, ukosefu wa makampuni kutozingatia wajibu wao juu ya haki za binadamu katika kipindi cha utekelezaji wa shughuli za usambazaji wa miundo mbinu ya umeme katika maeneo ya vijiji Pamoja na ukosefu wa juu ya uelewa wa wanainchi juu ya haki hizo katika maeneo ya vijijini kumepelekea kujikuta katika hali tete juu ya haki zao za msingi.

utafti huu umependekeza yafuatayo; 1) makandarasi na wadau wa serikali kuzingatia maswala ya haki za binadamu wakati wa kuunda miradi hiyo na pia kuhakikisha haki hizo zinaingizwa wakati wa usimikaji wa miundombinu ya nishati ya umeme 2) makandarasi waelekezwe namna bora ya kuheshimu haki za binadamu wakati wa utekelezaji wa kazi zao 3) sheria zitungwe na kusimamiwa ili kuhakikisha usimamizi wa haki za binadamu unatekelezwa kikamilifu na ufuatiliaji unaboresha, na 4) Watu wa vijijini wapatiwe elimu itakayo wawezesha kuongeza ufahamu juu ya haki zao, na kuelekezwa juu ya mahusiano yaliopo kati uendeshaji wa biashara za ukandarasi na wajibu wao wa kisheria katika kisimamia wajibu, kutambua, kupokea, kushughulikia na kuendesha mijadala ya kutafuta suluhu juu ya haki zilizovunjwa.

Kwa ujumla utafiti umependekeza kua ni lazima kwa kila mkandarasi/makampuni kua kwao ni lazima kuhakikisha usimamaizi bora wa haki za binadamu katika nyakati za utekelezaji wa shughuli zao. Hii itasaidia kuhakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa na wananchi wanalindwa ipasavyo.



### **Haki za binadamu na ushiriki wa raia katika Mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania: chunguzi kifani za Arusha na Dodoma (FEMAPO)**

*Mradi wa Kuendeleza Majiji ya Kimkakati Tanzania" (TSCP) ni mradi mkubwa wa maendeleo ya miundombinu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) na kutekelezwa na Serikali ya Tanzania. TSCP ililenga kuboresha miundombinu na huduma za miji katika majiji nane yanayokua kwa kasi nchini Tanzania, ambayo ni pamoja na Dodoma na Arusha. Mradi huo ulikuwa muhimu kwa jamii za Manispaa ya Arusha na Dodoma, kwani ingeleta maendeleo na usalama unaohitajika kwa vitongoji ambapo ulikuwa ukitekelezwa. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa TSCP inaleta mabadiliko chanya na hali bora za maisha kwa jamii zinazolengwa, lazima kuzingatia haki za msingi za binadamu katika utekelezaji wake. Kwa hiyo, katika utafiti huu, FEMAPO ililenga kuchunguza ulinzi wa haki za binadamu na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa mradi wa TSCP katika miji miwili: Arusha na Dodoma.*

Utafiti huu ulijaribu kutathmini mambo matatu kama ifuatavyo: (1) ushiriki wa raia na ushirikishwaji wa jamii, (2) athari za haki za binadamu, na (3) upatikanaji wa suluhisho au urejeshaji wa haki.

Matokeo ya utafiti wetu yanaonyesha kuwa mradi wa TSCP huko Arusha na Dodoma ulizingatia kiwango cha msingi cha ushiriki wa raia na ushirikishwaji wa jamii, ulinzi wa haki za binadamu na upatikanaji wa huduma za urejeshwaji wa haki, kama inavyotakiwa na miongozo ya benki ya Dunia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, juhudi bado zinahitajika kuboresha mchakato wa ushiriki na mashauriano ya wananchi kama njia ya kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu / kupunguza athari na ufikiaji mzuri wa suluhisho. Kama masuala muhimu, tumegundua: (1) ingawa mikutano ya ushirikishaji au mashauriano iliandaliwa, kulikuwa na kasoro katika kujumuisha makundi tofauti ya wadau; (2) ingawa hakuna madhara makubwa ya haki za binadamu yaliyoripotiwa, malalamiko yaliibuka kuhusu kiasi cha fidia kinachofaa pale palipokuwa na upoteaji wa mali kutokana na kazi za ujenzi wa TSCP huko Arusha; (3) ingawa utaratibu wa kupokea malalamiko ulikuwepo, ukosefu wa ufahamu na kutokuwa na namna rahisi kwa jamii kuwasilisha malalamiko yao kulizuia ufanisi wa mchakato huo.

Kwa jumla, matokeo ya utafiti wetu yanaonyesha kuwa ni muhimu kuijengea jamii uwezo wa kuelewa haki zao za msingi za binadamu na jinsi ya kutetea na kuzilinda haki hizi. Tunahitimisha kuwa ushiriki wa raia na ulinzi wa haki za binadamu ni mambo muhimu katika mradi wowote wa uwekezaji wa miundombinu.

Kulingana na utafiti huu, tunapendekeza Serikali ya Tanzania na wabia wake wa maendeleo (kwa mfano Benki ya Dunia) kuweka ulinzi wa Haki za Binadamu na Ushiriki wa Raia kama vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya miundombinu. Tunasisitiza pia hitaji la kuijengea jamii uwezo wa kuelewa na kutetea haki zao za msingi kama binadamu, na kuweka mfumo bora, wenye manufaa na ulio rahisi kufikika ili kushughulikia malalamiko ya jamii kwa ufanisi pale wanapoathirika na hatua za utekelezaji wa miradi hii.

Somo ambalo tumejifunza kutokana na mradi wa TSCP linapaswa kutumiwa kuboresha utekelezaji wa miradi mingine inayofanana na huu kwa siku zijazo.



## UTAFITI WA 5:



**Miradi mikubwa ya Miundombinu nchini Tanzania na Athari zake kwa Haki za Binadamu: Uchunguzi Kifani wa Mradi wa Ukarabati wa Reli ya Dar es Salaam-Moshi katika Wilaya za Mwanga na Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro (AJISO)**

*Tanzania, kama nchi nyingi zinazoendelea, inajitahidi kuongeza ukuaji wake wa uchumi wakati pia ikizingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG). Maendeleo ya Viwanda yanaonekana kuongoza ukuaji huu. Kama matokeo, miradi mingi mikubwa ya miundombinu inaendelea, kama vile kuboresha mifumo ya reli nchini.*

Katika kutekeleza miradi hiyo, nyanja za Haki za Binadamu mara nyingi hupuuza na pia kufuata vyombo vya kimataifa kama vile Kanuni za Uongozi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za

Binadamu (UNGP) za 2011 inaonekana kuwa changamoto. Kwa sasa, kuna ufahamu mdogo na taarifa za kina juu ya asili na ukubwa wa ukiukaji wa haki za binadamu nchini, haswa kuhusiana na maendeleo ya miundombinu. Utafiti huu uliundwa kushughulikia pengo hili.

Katika utafiti huu, tunaangaza ufufuaji wa mradi wa reli ya Dar es Salaam-Moshi kama utafiti wa athari za miradi mikubwa ya miundombinu juu ya haki za binadamu nchini Tanzania. Kufufuliwa kwa reli ya Dar es Salaam-Moshi ni moja wapo ya miradi mikubwa ya miundombinu ambayo imefanywa hivi karibuni nchini Tanzania. Kama miradi mengine mikubwa; athari mbaya za haki za binadamu zinawezekana, zikiathiri haki za wafanyakazi, haki ya kuishi salama na hali nzuri, haki za mazingira, na haki zinazohusiana na jinsia.

Utafiti huo unakusudia kutathmini kwa kiwango gani mradi wa ufufuaji wa reli ya Dar -es Salaam hadi Moshi ulizingatia viwango vya haki za binadamu na Kanuni za Uongozi za Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu haswa. Maswali muhimu kwa hivyo yalikuwa;

i) Je! ni haki gani za binadamu zilizokiukwa katika kutekeleza mradi huo?

ii) Je! ni hatua gani zilizochukuliwa na Serikali kulinda jamii na kuhakikisha kuwa haki za binadamu hazikiukwi wakati wa utekelezaji wa mradi?

iii) Je! Ni kwa kiwango gani jamii inayozunguka miradi hiyo ina uelewa wa haki zao na stahiki zilizopo ikiwa kutakuwa na ukiukwaji:

Utafiti huo ulifanywa katika Wilaya za Mwanga na Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro (Kaskazini Mashariki mwa Tanzania). Jumla ya watu 40 (23 wa kiume, 17 wa kike) walihojiwa. Njia nyingi za utafiti zilitumika, pamoja na mahojiano ya simu / mtandaoni na mahojiano ya mtu mmoja mmoja, kwa sababu ya janga la COVID-19 na hatua za kuzuia kuenea kwa ugonjwa huu.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa baadhi ya ukiukaji wa haki za binadamu ulioripotiwa katika ukarabati wa reli ya zamani ni pamoja na ukiukaji wa haki za kazi kama vile hali mbaya ya kufanya kazi, mishahara midogo na masaa marefu ya kazi; kutokea kwa ajali ambazo zilisababisha vifo na majeruhi ya watu na mifugo; mmomomyoko wa udongo; kuzuka kwa magonjwa ya kuambukiza na ya zinaa na migogoro ya kifamilia kama vile kuvunjika kwa ndoa na ujauzito wa watoto.

Mradi huo pia ulileta athari chanya, haswa faida za kiuchumi na ajira. Faida zilizotajwa ni pamoja na kupunguzwa kwa gharama za usafirishaji, kuongezeka kwa uwezekano wa kibiashara, na kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana na wanawake, kuongezeka kwa faida ya mtaji pamoja na kuongezeka kwa aina mbalimbali za shughuli za kiuchumi.

Kuhusu upatikanaji wa fidia ikiwa kuna ukiukwaji wa haki, iligundulika kuwa ni 15% tu ya wahojiwa walisema kufahamu haki zao kuhusu fidia na stahiki ikiwa haki zao zitakiukwa wakati wa miradi ya ujenzi au shughuli zingine za maendeleo.

Kwa ujumla, utafiti huu umeona kuwa hatua kadhaa ziliwekwa ili kuhakikisha kuwa kuna ufuatiliaji, heshima na ulinzi wa Haki za Binadamu katika miradi mikubwa ya maendeleo. Walakini, hatua zilizochukuliwa hazikutosha kuhakikisha ukiukaji wa haki za binadamu uliepukwa wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Kwa hivyo, ni muhimu kwamba Serikali na washirika wake waongeze juhudi zao za kukuza uelewa juu ya majukumu, haki na fidia zilizopo endapo kutakuwa na ukiukwaji wa haki wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Kanuni za Uongozi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu zinaweza kuwa nyenzo ya kuongoza njia ya kusonga mbele.

## HITIMISHO JUMUISHI NA MAPENDEKEZO

Tafti tano zilizowasilishwa katika toleo hili la tatu la “*Sauti za Watanzania*” zililenga **athari za miradi mikubwa ya miundombinu kwa haki za binadamu** ambayo inaendelea au imekamilika hivi karibuni katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Dodoma ya Tanzania. . Utafiti huo ulilenga aina mbili za miradi ya miundombinu: zile zinazotoa **usambazaji wa nishati** (Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Mradi wa Umeme wa Umeme wa Rusumo Falls na miradi ya usambazaji wa nishati vijijini) na zile zinazopeleka **miundombinu ya uchukuzi** (mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania na Reli ya Dar es Salaam - Moshi).

Tafti hizi ziliongozwa na maswali yaliyohusu (1) **utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu** unaotakiwa kufanywa na makampuni, (2) **athari** za miradi maalum ya miundombinu **kwa jamii**, (3) **upatikanaji wa fidia** endapo kuna ukiukwaji wa haki za binadamu, na (4) **uhusishwaji, ushiriki na uhamasishwaji** wa jamii katika maendeleo ya miundombinu na haki za binadamu.

Njia mojawapo ya kutathmini kama na jinsi shughuli za biashara zinaheshimu haki za binadamu, ni kupitia **michakato ya utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu**. Kimsingi, kutambua athari hasi na kuleta ufumbuzi wa kutosha kupunguza athari hizo ni sehemu ya mchakato wa tathmini ya hatari ya makampuni. **Katika tafti nyingi zilizowasilishwa kwenye toleo hili aina fulani ya tathmini juu ya hatari / athari ilifanywa kiundani**. Hii ilifanywa ama kwa kufuata sheria za Tanzania - k.v. Mahitaji ya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA), kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004- au kwa kuzingatia mahitaji maalum ya wafadhili - mf. uchunguzi wa Mfumo wa Mazingira na Jamii wa Benki ya Dunia (ESF). Ni muhimu kujua kuwa hakuna tathmini hata moja kati ya hizi inafikia utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu kwa kuzingatia “jicho la haki za binadamu”, kama inavyopendekezwa na Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu<sup>11</sup>. **Wakati tathmini nyingi za hatari na mipango ya kupunguza inakaribia kukamilika, kuna mapungufu yamebainika**. Haya yanaonekana kuhusishwa na ukosefu wa maarifa ya kina ya muktadha mgumu na mahususi wa maeneo husika, ushiriki hafifu na mazungumzo na wadau, na mchakato ya utekelezaji wa haki za binadamu kutokamilika Kutokana na ukweli kwamba hakuna hata moja ya tathmini hizi inayochambua athari hasi zinazoweza kutokea kwa upande wa ukiukwaji wa haki za binadamu hiyo inasababisha ugumu mwingine mkubwa.

Uelewa mdogo wa muktadha wa mahali husika unaweza kusababisha mali za jamii, iwe ardhi ya jadi, mali, maisha / mazoea ya kiuchumi, maeneo ya kiutamaduni au majukumu ya jamii, kuchukuliwa kuwa “rahisi kufidiwa” na “athari ndogo” za hasara zao, wakati kiukweli ni kubwa. Kwa mfano, uchunguzi kifani wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) linalopita kwenye jamii za wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Kiteto (Manyara). Utafiti huo unatoa mifano mbalimbali ya jinsi **uelewa wa kina zaidi wa muktadha unahitajika ili kulinda jamii, maisha yao na mila zao**. Inaonyesha pia kwamba sio vyote vinavyopotea vinaweza kubadilishwa au kufidiwa kirahisi, kama inavyodhaniwa mara nyingi. Katika mfano mwingine, utafiti juu ya ukarabati wa reli ya Dar es Salaam hadi Moshi katika mkoa wa Kilimanjaro, unaonyesha kuwa hatua za kupunguza athari zinaonekana kulenga tu masuala ya usalama, lakini zilipuuza athari zingine kama vile mazingira, afya au masuala ya kazi. Utafiti wa Mradi wa Umeme wa Maji wa Maporomoko ya Rusumo (RRFHP), uliotfanyika katika mkoa wa Kagera, unaonyesha kuwa

11 Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji wa Mfumo wa ‘Kulinda, Kuheshimu na Kupata Unafuu wa Kisheria’, Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR); 2011. [https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR\\_EN.pdf](https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR_EN.pdf)

wahusika wa RRFHP waligundua athari muhimu wakati wa tathmini zao juu ya hatari. Hata hivyo, walishindwa kuwa na ufanisi kwenye hatua zao za kupunguza athari hizo. Hii imesababisha jamii kushughulikia athari hasi tu za mradi, kama uchafuzi wa hewa au maji.

Ushiriki na mazungumzo na wadau ni vitu muhimu katika michakato ya utekelezaji wa haki za binadamu na inaweza kuwa chombo chenye nguvu kuhakikisha kuna kutambua vema, kuzuia na kupunguza hatari. **Katika tafiti zote tano, kiwango fulani cha ushirikishwaji jamii kilifanyika**, haswa kabla ya utekelezaji wa kazi za miundombinu. Upeo, mzunguko na ukubwa wa mikutano hii ulitofautiana, kutoka kwa ushiriki wa dharura wa viongozi wa vijiji katika masuala ya utekelezaji, hadi mikutano ya uhamasishaji wa usalama kwa jamii au mazungumzo ya mara kwa mara kati ya watekelezaji wa miradi, viongozi wa serikali za mitaa na wanajamii walioathiriwa. Pamoja na hayo, tafiti nyingi zinahitimisha kuwa **ushiriki huu haukutosha kuhakikisha kuna mazungumzo na ushiriki wa kweli wa jamii**. Zinaonyesha pengo la utekelezaji kati ya mipango na mazoea ya kampuni kuhusu ushiriki wa jamii. Ugunduzi muhimu ni kwamba ufuatiliaji kwa wadau (jamii) unaonekana kwa kiasi kikubwa haupo na **maarifa na ufahamu juu ya jinsi miradi ya miundombinu inaweza kuathiri jamii na haki zao bado ni mdogo sana**. Ukosefu huu wa ufahamu unawaacha watu kwenye hatari ya kutotendewa haki.

**Athari za haki za binadamu za miradi mitano ya miundombinu** iliyowasilishwa hapa ziko zaidi kwenye haki za kiuchumi (k.m. fursa za kujipatia riziki), haki za wafanyakazi (k.m. mazingira ya kazi), afya (k.m. mlipuko wa magonjwa), mambo ya kijamii na kiutamaduni (mfano tamaduni za jamii) na haki za mazingira (mfano uchafuzi wa mazingira, mmomonyoko wa udongo, kuwa na mifumo ya kiikolojia). **Ingawa athari nyingine ni hasi kabisa, sio zote ziko hivyo**. Miradi kama RRFHP, Mradi wa Miji ya Kimkakati ya Tanzania (TSCP) au ukarabati wa reli ya Dar es Salaam - Moshi imeleta ajira na fursa za biashara kwa jamii, mbali na miundombinu iliyoboreshwa. Tafiti kadhaa zinaonyesha uhusiano kati ya miradi ya miundombinu na haki za ardhi<sup>12</sup>, sio kidogo kuhusu masuala na fidia isiyo ya haki kwa ardhi na rasilimali zilizopotea kuwezesha maendeleo ya miundombinu.

Fidia ni mojawapo ya njia zinazojulikana zaidi za kuleta ufumbuzi wa jambo. **Kampuni kuheshimu haki za binadamu pia kunahitaji kupata ufumbuzi madhubuti**, i.e. kuwepo kwa mifumo na taratibu ambazo zinaruhusu watu kutoa kero zao na kupata ufumbuzi bora za athari hasi. **Miradi kadhaa ya miundombinu iliyotafitiwa kwenye toleo hili ni pamoja na utaratibu wa malalamiko**. Miradi ya EACOP, RRFHP na TSCP ina taratibu za hali ya juu zaidi za kushughulikia malalamiko ya watu walioathirika. Hata hivyo, licha ya uwepo wa madawati ya malalamiko, ofisi za uhusiano na utatuzi wa migogoro au kamati za usimamizi wa miradi ya jamii, **wanajamii hawajaridhika, hawaamini au hawajui uchaguzi uliopo kwa ajili yao**. Kama mtoa taarifa mmoja kutoka Wilaya ya Kiteto alivyofafanua *“aliyetupa mchakato wa malalamiko ndiye tunamlalamikia”*<sup>13</sup>. Shuhuda nyingine zinataja ukosefu wa majibu ya wakati unaofaa au ya wazi kwa malalamiko yaliyowasilishwa, mikataba ya fidia isiyo ya haki, urasimu mkubwa, ukosefu wa ushirikiano mahali husika kwa kuwasilisha malalamiko au kutokujua kabisa taratibu na haki. **Kwa hiyo, upatikanaji wa mifumo madhubuti ya malalamiko kwa sasa unaonekana ni mdogo**. Kwa kweli, kama inavyoonyeshwa na Umoja wa Mataifa<sup>14</sup>, utaratibu mzuri wa malalamiko wa kampuni unapaswa kuwa halali, upatikane, utabirike, uwe wa wazi, wenye usawa, wenye haki sawa, chanzo cha mafunzo endelevu na wenye msingi wa ushiriki na mazungumzo.

Mwisho, chunguzi kifani kwenye toleo hili la tatu la *“Sauti za Watanzania”*, zinasisitiza **umuhimu wa kukuza uelewa, michakato ya ushiriki na mazungumzo na wadau** kama vitu muhimu vya kutetea haki za binadamu na uwajibikaji wa makampuni. Hizi zinapaswa kuwa zaidi ya “mazoezi mazito” na badala yake ziunde mawe ya msingi ya michakato ya utekelezaji wa dhati wa haki za binadamu. Chambuzi za shughuli za biashara katika mfumo wa haki za binadamu zinaweza pia kuashiria maendeleo makubwa. Hata hivyo, kwa sasa michakato inayolenga haki za binadamu inabaki kuwa mipango ya hiari katika sekta na nchi nyingi. Miradi mikubwa ya maendeleo, kama vile miradi mikubwa ya miundombinu iliyotafitiwa kwenye toleo hili, bila shaka itaathiri haki za msingi za wengi. **Kufanya haki za binadamu**

12 Tafiti zaidi zinazohusu masuala ya haki za ardhi na za binadamu, zinapatikana kwenye toleo la pili la “Sauti za Watanzania”: <https://ipisresearch.be/publication/voices-tanzania-case-studies-business-human-rights-vol-2-land-rights-environment/>

13 Angalia utafiti uliofanywa na Shirika la Maendeleo ya Gesi (PILIDO).

14 Miongozo ya Umoja wa Mataifa juu ya Biashara na Haki za Binadamu: Utekelezaji wa Mfumo wa ‘Kulinda, Kuheshimu na Kupata Unafuu wa Kisheria’, Ofisi ya Kamisheni Kuu ya Haki za Binadamu (OHCHR); 2011. [https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR\\_EN.pdf](https://www.ohchr.org/Documents/Publications/GuidingPrinciplesBusinessHR_EN.pdf)

**kuwa za lazima kwenye biashara, badala ya hiari**, kutakuwa hatua muhimu ya kuhakikisha haki za binadamu zinazingatiwa vya kutosha katika shughuli za makampuni na maendeleo yanafanyika kupitia makampuni kuheshimu haki za binadamu.

Ripoti kamili za chunguzi kifani hizi zinapatikana kwa Kiingereza kupitia <https://ipisresearch.be/home/capacity-enhancement/voices-from-the-south/voices-from-tanzania/>



“Sauti za Watanzania” ni ushirikiano baina ya asasi za kiraia za Tanzania, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BHRT) na Shirika la IPIS. Chapisho hili ni sehemu ya mradi wa ‘Uboreshaji wa ufuatiliaji, tafiti na majadiliano juu ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania’ unaotekelezwa na CHRAGG, BHRT na IPIS, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Kitengo kinachoshughulikia Demokrasia na Haki za Binadamu (EIDHR).

Mawasiliano: bizhumanrightstanzania@gmail.com